# Bure bora?




Jishindie kompyuta ndani!

Kijitabu hiki kimetayarishwa na watendaji wa Tamasha kwa kushirikiana na Twaweza

Waandishi:
Richard Mabala na Winston Churchill Shauri

Mchoraji:
Daniel Mzena

Wahariri:
Rakesh Rajani, Evarist Kamwaga, Joseph Ngwegwe na
Justice Rutenge

Usanifu:
Winston Churchill Shauri

©Tamasha/Twaweza 2012

Barua: S.L.P. 15044, Arusha, Tanzania
Simu: +255 719 751 928
+255 787 220 233

Barua pepe: rmabala@yahoo.com
wchachi@yahoo.com

Tovuti: www.tamashavijana.org

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kijitabu hiki kwa sababu zisizo za kibiashara tu. Unachotakiwa kufanya ni kunakili chanzo cha sehemu uliyonakilia na kutuma nakala mbili kwa Tamasha.

## Utangulizi

Ndugu wasomaji,

Afya ya msingi ni msingi wa maisha yetu. Serikali imejitahidi sana kupanua huduma za afya hadi vijijini. Aidha Sera ya Afya ya Taifa imetambua vikundi maalum, kama vile wanawake wajawazito, watoto wadogo, watu wenye magonjwa ya kudumu na wazee kwamba wanastahili kupewa matibabu bila malipo. Mafanikio hayo na dhamira hizo za serikali zinastahili pongezi sana.

Hata hivyo, utekelezaji, una matatizo makubwa.

- Licha ya kutamka mara nyingi dhamira ya kuhakikisha kwamba 15% ya bajeti inaenda kwenye sekta ya Afya ifikapo 2015, mwaka 2011 bajeti ya Afya imeshuka hadi 8.8% ya bajeti ya taifa (kutoka 11%).
- Ingawa zahanati na vituo vya afya vimeongezeka sana, bado kuna uhaba mkubwa wa wafanyakazi wa afya. Hadi sasa, hawafikii hata nusu ya wafanyakazi wanaohitajika.
- Wafanyakazi wa afya wengine hawafuati maadili ya kazi yao, ama kwa kukasikirikia hali duni ya mapato na mazingira ya kazi, ama kwa sababu hawafuatiliwi na kuwajibishwa.
- Sehemu nyingi wanawake wanaotaka kujifungua wanaambiwa lazima waje, si na vifaa vyao tu bali hata maji yao na taa pamoja na kununua dawa. Asiyeleta hapati huduma.

Kwa hali hii, ni muhimu jamii ishiriki katika kuboresha vituo vilivyopo pamoja na miundombinu ili kurahisisha kufika kwenye vituo. Aidha kamati za afya za kata, ziwakilishe kweli watumiaji wa huduma za afya na kufuatilia utoaji huduma.

Hali ikoje kwenu?

Richard Mabala
Mkurugenzi, Tamasha

# Wahusika



**Bonge:** Mjasiriamali, mchambuzi wa mambo na mkereketwa wa maendeleo



**Bibiye:** Mwelimishaji rika, mchambuzi na mwanaharakati



**Mwenyekiti:** Kiongozi anayesikiliza na kuheshimu vijana. Mpenda maendeleo lakini anaamini zaidi msaada kutoka nje kuliko nguvu ya wananchi



**Mtendaji:** Mchapakazi lakini mrasimu. Hapendi vijana na azma yao ya kuchukua hatua wenyewe



**Mawazo:** Kijana, rafiki wa Bonge na Bibiye



Jamani nitapata wapi? Nakaa peke yangu.
KITUO CHA AFYA
HUDUMA BURE KWA WANAWAKE WAJAWAZITO NA WATOTO WADOGO
Tumekuambia bila vifaa haingii mtu hapa.
!
Yatuhusu nini? No vifaa! No kujifungua hapa!


Mapenzi raha mimba karaha ha! ha! haa!
TUO CHA AFYA
Aaaaa...
Dadaaa...
Eti! Tulikuwepo wakati wa raha zake? He! he! he!


Nyumbani kwa Bonge
Zinduna yuko wapi sasa? Hata kupiga simu?
Tulia kaka. Si ulisema chaji ya simu imeisha. Angejaza wapi?
Ah! umeme noma, simu hamna, barabara hovyo, kituo cha afya mbali, mambo gani haya?


Ghafla...
Amekufa jamani, amekufa jamani... eeee...!
Nani? Fadhila?
Hapana ni mtoto wake. Kwani wale wauguzi wahuni walijali!


Nilikimbia mjini kupata vifaa vya uzazi. Niliporudi Fadhila alikuwa tayari lakini mtoto...
! !
Fadhila mwenyewe kanusurika. Walimwacha ajifungue peke yake.




Makaburini


Nyumbani kwa Zinduna
Nimesema zahanati siendi tena. Mara kumi kwa mkunga wa jadi.
Lakini ni kwa usalama wako.
Jamani, ubishi huohuo kila siku?
Mwambie! Anashikia bango utadhani Zahanati ni mali yake.


Lakini dada, ni bora uende kliniki. Wafanye vipimo.
Ohooo! Yaleyale. Kliniki nitaenda lakini kujifungua... thubutu!


Lakini nasikia kuna semina ya akina mama leo.
Ndiyo. Mama Afya wa wilaya amekuja. Wanawake wajifungue kwenye kituo cha afya si nyumbani.
Weeee! Ngoja twende. Nakuambia leo hapatoshi.


Mkutano wa kijiji
Akina mama tutumie haki zetu. Sera yetu ya afya inasema huduma za uzazi ni bure, mnangoja nini?
Ni bure kwelikweli. mtoto kafariki juzi kwa uzembe tu.


Si kweli, vituo vyetu ni salama lakini mara nyingine ni mipango ya Mungu.
Mungu anapanga uzembe? Na matusi?
Na hata kama hakuna malipo, bila kwenda na vifaa mwenyewe, hupati huduma


Kama kuna makosa ya aina hiyo tutachukua hatua.
Makosa yapo tele, Fanyeni uchunguzi. Na tuone hatua. Ahadi ni...
Deni...! deni...!


Baada ya wiki mbili
Unaona mwenyekiti? Hadi sasa hakuna lolote lililofanyika.
Dawa ni kuwa na Zahanati yetu. Lakini nyinyi vijana hamtaki kuifanyiakazi.
Waambie Mwenyekiti. Hawa mpaka wabembelezweeee utadhani waheshimiwa wa posho.


Siyo kubembelezwa. Jengo pekee si zahanati.
Na la muhimu ni ukaribu wa jengo au ubora wa wahudumu?
Barabara nzuri na usafiri ndio muhimu.
Huduma itakuwa bora ikiwa karibu.


Tena tukijenga, serikali itatupatia wahudumu wa afya.
Wahudumu au wahujumu? Angalia yaliyompata Fadhila.
Na watapatikana wapi? Hawatoshi nchi nzima.


Vijana wakikusanya maoni
Na vipi Walikujali?
Ah! wapi! matusi matupu.
Ulilipa chochote?
Ndiyo. Shilingi elfu mbili kwa ajili ya dawa.


Kwenye kituo
Sasa watabisha nini? Wakina mama 30 kati ya 40, walilazimika kulipa au kuja na vifaa vyao.
Na tuna kurasa tatu za matusi yaliyotolewa. Mpaka nimejifunza mengine.


Angalia huo ushahidi mwenyekiti. Inatosha kabisa kuwaambia wabadili tabia.
Nyie vijana hatari sana. Tayari mmeshamaliza?


Itabidi nipeleke kwa mtendaji kata, pia nimshauri tuwe na kamati ya afya ya kata.
Matatizo ni mengi. Dawa zenyewe hakuna zaidi ya Panado na kondomu.
Eti huduma za bure wakati mgonjwa lazima aende hata na maji yake na taa yake.


Baada ya wiki moja. Nje ya kioski cha Bonge
Nina habari njema. Mtendaji Kakubali.
Kweli?
Sasa tuanze kazi.
Kwanza akasema nyinyi vijana wakorofi lakini angebisha nini?


We mangi hebu lete mchango wa umeme wa jua. Mama zetu wajifungue. kwa raha.
Bonge umekuwa mwenyekiti wa kijiji? Ha! ha! haa! Haya baba yangu. Kweli umeme ni maendeleo.


MAWAZO
YA NINI
AMBULANCE
Eti kituo Chetu hakijapangiwa bajaji. Nitatengeneza mwenyewe.
He mjasiriamali! Kwa pamoja...


Usiwe na wasiwasi dada. Mtoto amekaa vizuri. Lakini chukua hizi dawa kama tahadhari.
KITUO CHA AFYA
Asante dada.
HUDUMA BURE KWA WANAWAKE WAJAWAZITO NA WATOTO WADOGO
Kama mambo ndiyo hayo, hata mimi nitakuja hapa kujifungua.

## Je wajua?

**Vifo na magonjwa ya uzazi**

1. Wanawake wajawazito wanashauriwa kuhudhuria kliniki mara nne kabla ya kujifungua na pia kujifungua kwenye kituo cha afya huku wakihudumiwa na mtu aliyesomea afya.
2. Ingawa karibu wanawake wote wanahudhuria kliniki angalao mara moja, chini ya nusu wanaenda mara nne. Idadi hii imeshuka sana kutoka 63% (2005) hadi 43% (2010).
3. Nusu tu ya wanawake wanajifungua kwenye kituo cha afya na kuhudumiwa na mhudumu wa afya aliyesomea kazi hii. Huko vijijini ni 42% tu.
4. Hali hii huchangiwa na umbali wa vituo vya afya, na hali ya huduma.
5. Kuna upungufu mkubwa sana ya wafanyakazi wa afya (65%)[1]. Itachukua miaka mingi kuondoa upungufu huo, bila hata kuongeza idadi ya zahanati na vituo vya afya kulingana na sera inavyosema.
6. Vifo vya uzazi ni 17% ya vifo vyote vya wanawake kati ya miaka 15 na 49.
7. Kila kijiji kinatakiwa kuwa na kamati ya afya itakayoshirikiana na Kamati ya Maendeleo ya Kata kufuatilia masuala ya afya katika mipango ya kata pamoja na utoaji wa huduma za afya.

**Tufanye nini?**

- Wanaojua zaidi tufanye nini ni wanawake na wasichana. Tumewauliza?
- Ufuatiliaji huongeza uwajibikaji. Ukurasa wa 27 wa kijitabu hiki kuna mfano wa maswali ya ufuatilijiaji.
- Wakunga wa jadi wameshirikishwa vipi katika kulinda afya ya mama na mtoto? Na kupewa nyenzo na mafunzo?
- Tunashiriki vipi katika kamati ya afya? Tumewakilishwa sawasawa?

---

1 HSSPIII 2009

**Mimba za umri mdogo**

- Wanaopata mimba na kujifungua kabla ya kufikia miaka ishirini wako hatarini zaidi kuugua au kufa, pamoja na watoto wao.
- Asilimia tano ya wasichana wameshapata mimba kufikia miaka 15 na 44% kufikia miaka 19. Karibu 40% ya wanawake wameolewa kabla ya kufikia miaka 18. Lakini sehemu nyingi hakuna huduma maalum inayozingatia matatizo ya kipekee ya wanawake wa umri huo[1].
- Katika tafiti zilizofanywa na TAMASHA, vijana wengi hawawezi kupata njia za kupanga uzazi kwa njia rasmi. Hivyo wanatumia njia zisizo rasmi bila ushauri wala kupimwa kuona njia zipi zinawafaa.
- Tafiti kote duniani zinaonyesha kwamba kuwaelimisha vijana kuhusu afya ya uzazi na ujinsia hakuongezi vitendo vya ngono bali kunapunguza. Elimu hujenga mahusiano na vitendo bora zaidi.

**Tufanye nini?**

- Ili kuzuia mimba za umri mdogo, tuwe wazi na vijana wetu. Pawe na mipango ya kutoa elimu ya masuala ya afya ya uzazi na ujinsia.
- Pawe na mjadala wa wazi kuhusu uzazi wa mpango kwa vijana ili kuwakinga wasichana wasipate mimba kwa wakati usiofaa lakini kwa kuzingatia afya zao na maadili.
- Vijana kwa kushirikiana na uongozi waweke mpango wa ulinzi wa wasichana.

---

1 Takwimu hizo zinatoka TDHS (2010) isipokuwa pale ambapo chanzo kingine kinatajwa




## Hali ikoje kwenu?

Hata wewe na wenzio mnaweza kupima hali halisi ya huduma za afya, (kwa kushirikiana na kamati ya afya na wengine) kama walivyofanya vijana katika kijitabu hiki. Baadhi ya maswali ya kuuliza ni kama:

- Je umeridhika na huduma ulizopewa? Kwa nini?
- Ilibidi ulipie kitu chochote? Kitu gani?
- Uliridhika na kauli za wahudumu?
- Dawa zilipatikana?
- Kama hazikupatikana uliambiwaje?
- Ulipewa maelezo ya kutosha kuhusu jinsi ya kutumia dawa hizo?
- Ulitakiwa kupimwa? Vipimo vilikuwepo?
- Walikuwepo madaktari/manesi wangapi?

**Shindano**

# *Toa maoni, jishindie kompyuta!*

Ndugu msomaji, hivi karibuni Serikali ya Tanzania imeahidi kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

**Kupitia mpango huu, Serikali inataka kukusikia.**

Toa maoni yako kuhusiana na upatikanaji wa huduma za msingi za kijamii; maji, elimu na afya.

***Tuambie wazo moja kuboresha elimu, afya au maji. Halafu, tuambie mwananchi afanye nini kuleta mabadiliko.***

Kila baada ya miezi mitatu kwa mwaka 2013, maoni kumi bora yatachaguliwa na kila shule itakayotoa washindi itapatiwa kompyuta ndogo mbili (laptops). Pia, maoni ya washindi yatachapishwa kwenye vitabu na tovuti.

**Sharti:** Kila mtu anaweza kutuma maoni, lakini zawadi zitatolewa kwa watakaondika *kupitia* shule zao tu.

**Tuma maoni yako kabla ya tarehe 1 Novemba, 2013**

**Anuani:** OGP Tanzania, S.L.P 38342, Dar es Salaam

**Barua pepe:** unasemaje@gmail.com

**Kumbuka kuweka taarifa hizi:**

- Tarehe
- Majina kamili, umri wako, jina la shule; jinsia (me/ke)
- Anuani kamili: SLP na makazi (kata, wilaya na mkoa); namba ya simu; barua pepe

## *Mpango wa Kimataifa wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi* (Open Government Partnership - OGP).

Mpango wa OGP unahimiza shughuli za Serikali ziendeshwe kwa uwazi zaidi ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, mwitikio wa Serikali, kupambana na rushwa na kujenga kuaminika zaidi. Twaweza inashirikiana na Serikali kuendeleza uwazi na ushiriki wa wananchi kupitia Mpango wa OGP.